EAF·PAM
PL8704
·R59H3

# DITHI ZA RAFIKI SABA

R. L. RIWA



HAZINA YA MAANDISHI
YA
AFRIKA YA MASHARIKI

## DIBAJI

kwa

## HAZINA YA MAANDISHI YA AFRIKA YA MASHARIKI

*

Mataifa yote ya ulimwengu huwa na kitu chenye thamani kubwa; kitu hicho ni hazina ya mambo ya kabila —hadithi, nyimbo, mithali, masimulizi ya mambo ya zamani za kale, na kadhalika; na hayo yote yanarithiwa kizazi kwa kizazi.

Mataifa ambayo yamezoea kuandika tangu zamani yanahifadhi hazina hiyo kwa kuandika na kupiga chapa vitabu vyenye mambo hayo. Wengine huandika na wengine husoma; hivyo, basi, kizazi cha wakati fulani hurithi kwa kizazi kilichotangulia. Ndivyo ilivyokuwa huku Afrika ya Mashariki, kabla Wazungu hawajafika, isipokuwa Waarabu na Waswahili walikuwa wameanza kuhifadhi mambo yao kwa kuandika wakitumia herufi za Kiarabu; mataifa mengine yalikuwa yakichukuliana mambo hayo kwa kusimuliana tu.

Siku hizi yametokea mabadiliko mengi katika maisha ya makabila ya Afrika karibu yote; hakuna nafasi ya kusimuliana kama zamani, na kwa sababu hiyo mambo mengi yanataka kusahauliwa. Yakisahauliwa, hazina hiyo ya mambo ya kikabila itapotea, na taifa lisilo na hazina hiyo ni maskini kweli.

Jamii hiyo ya vitabu inayoitwa TREASURY OF EAST AFRICAN LITERATURE (yaani HAZINA YA MAANDISHI YA AFRIKA YA MASHARIKI pamoja na jamii nyingine za HISTORY, FICTION (yaani NGANO), CUSTOM AND TRADITION (yaani DESTURI NA MASIMULIZI), imeanzishwa ili wazee na vijana wapate kushirikiana katika kuandika mambo ya taifa lao na kuhifadhi hazina yenye mambo ya kale na ya sasa ambayo ni urithi wa vizazi vya siku zijazo.



## YALIYOMO

*


| | ukurasa |
|---|---|
| Foreword (ya Kiingereza) ..... | ii |
| Dibaji (Kiswahili) ..... | iii |
| Utangulizi habari za Rafiki Saba ..... | 1 |
| Hadithi ya Ibrahim ..... | 3 |
| Hadithi ya Kombo ..... | 11 |
| Hadithi ya Samweli ..... | 15 |
| Hadithi ya Yakubu ..... | 24 |
| Hadithi ya Ɗaudi ..... | 31 |
| Hadithi ya Musa ..... | 36 |
| Hadithi ya Yohana ..... | 40 |
| Mwisho ..... | 43 |

## 1. HADITHI YA IBRAHIM

*Wakati Ibrahim alipotoa hadithi hii alimwelekea yule kijana, jina lake Daudi. Sababu yake ya kumwelekea hivi ni ya kuwa huyo Daudi alikuwa kijana mwenye udadisi kidogo, hata siku ile saa za mchana alikuwa amewasumbua wenzake kwa kuulizauliza maswali yasiyokuwa na maana sana. Lakini hata hivi walimpenda, maana alikuwa na bidii nyingi.*

# YALIYONIPATA PANGONI

## HABARI ZA WATOTO WATUKUTU NA MZEE MKALI

Karibu ya nyumba nilipolelewa na mama yangu kulikuwako mapango yaliyochimbuliwa zamani za kale ili watu wetu wapate kuyakimbilia na kujificha na adui wakati wa vita. Nilipokuwa mtoto mdogo nilikuwa na udadisi (hapo Ibrahim alimwelekea Daudi) nami nilikuwa na hamu sana ya kuyaingia na kuona kama kuna kitu ndani. Basi nilikuwa nikiulizauliza jamaa zangu habari za mashimo hayo.

Hata siku moja nikaenda msikitini pamoja na kaka yangu na watoto wengine. Tulipotoka nikasikia kuwa wenzangu wanakwenda kutazama pango moja lililokuwa karibu. Nikaomba wale wakubwa wangu waniruhusu niende nao. Wakesema. "Ye yote atakaye aweza kutufuata". Tukaenda watoto kumi na wawili, wengine wakubwa wengine wadogo. Mimi pamoja na watoto wengine watatu tulikuwa wadogo kuliko wote.

Tulipofika nyumbani kwa yule mwenye shamba lililo na pango tulimkuta mkewe tu, na bwana alikuwa hayuko. Tukamwomba mkewe aturuhusu kuingia pangoni akakataa akisema, "Bwana wangu hataki mtu ye yote aingie pango hili". Tukazidi kumwomba mpaka akakubali akisema, "Kama mjuavyo bwana wangu ni mkali sana, nami sitaweza kupigwa kwa ajili yenu. Mkitaka kuingia, ingia tu. Lakini, kama bwana wangu akija kabla hamjatoka nitamwambia kwamba ninyi mliingia kwa nguvu bila ruhusa yangu. Mkikubali hivyo, ingieni. La sivyo nendeni zenu, msiendelee kunisumbua." Tukamshukuru tukaenda kule kwenye pango.

Pango lile lilikuwa mwanzo wake ni shimo lililochimbwa ndani ya nyumba. Nyumba ilipochakaa ikaondolewa, na pango likawa wazi. Yule mwenyewe alikuwa